



Uwezesaji & Uhamasishaji wa wakulima wadogo wa mboga mboga Tanzania

«Anzia Sokoni Malizia Shambani Kwa Kipato Zaidi»

Muda:

Miaka 5
(Jan. 2019 – Dec. 2023)

Maeneo makuu lengwa:

Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, and Tanga.

Wanufaika :

~Makadilio. Kaya 4,000

Watekelezaji:

Wizara ya Kilimo na TAMISEMI*
Watendaji Kazi ni Kikosi kazi cha DADP**

Dhumuni:

Kufanya DADPs zifanye kazi ili kufanikisha mapato makubwa kwa wakulima wa mbogamboga kuitia mbinu za SHEP.

Mawasiliano:

Eng. Apolinary Kahabi Medard
JICA-TANSHEP Focal Point
Kilimanjaro RAS Office

kahabit@gmail.com

Mr. Mukara Mugini

PO-RALG,

mukara2002@gmail.com

Ms. Vumilia Nzinkakuba, MoA
vumilia.zikankuba@kilimo.go.tz

* Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

**Inausisha Idara ya sera na Mipango (DPP),
Idara ya Uratibu wa Sekta (DSC), Idara ya Maendeleo ya Mazao (DCD), Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC),
Horti. Tengeru, na Tanzania Horticulture Association (TAHA)

SHEP huanza na "Utafiti wa Soko" hufanywa na wakulima. Baada ya kugundua mahitaji ya soko, wakulima watakuwa wako kimkakati kupanga mpango wao wa uzalishaji ili kuongeza faida. Hii ni pamoja na kuchagua mazao / aina, ubora wa mazao / muda wa kuvuna nk.


Mradi wa Kuimarisha Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya na Uwezo wa Utekelezaji kwa kutumia mbinu ya SHEP (TANSHEP)



(Picha: Utafiti wa soko uliofanywa na wakulima)

Serikali ya Tanzania na Washirika wa Maendeleo (DPs) wamekuwa waktekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP) tangu mwaka 2003/04. Katika ASDP, kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGA) inaunda na kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADP), kuendana na eneo.

Mradi unakusudia kuimarisha uwezo wa Halmashauri kwa kuunda na kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADP) kwa kuanzisha mbinu ya SHEP. Hivi sasa, wakulima wengi wa mazao ya mbogamboga wanalima bila kujua mahitaji ya soko. Mara nyingi husababisha kuuza mazao kwa bei ya chini au hata mazao mengi Kutouzika. Kupitia SHEP, vikundi vyta wakulima vitabadilishwa kufuata "Kilimo kinacholenga Soko" na kuonyeshwa fursa nyingi (k.m. kutambulishwa kwa wanunuzi, wasambazaji pembejeo, taasisi za kifedha n.k. tofauti tofauti) kwa kuboresha mpango wa uzalishaji ili kupata faida kubwa.



* Kipeperushi hiki kimetengenezwa upya mnamo Agosti 2020, kuonyesha shughuli za kipindi cha 2019-2020

Utafiti wa Soko kwa wakulima



"Kabla ya TANSHEP sikuweza makubaliano ya bei ya mazao kwani sikujua mchakato wa uuzaaji. Lakini sasa nadhani naweza kuuza kwa bei kubwa zaidi kuliko hapo awali. Ninapanda mazao nikijua wanunuzi na bei ya soko. " - Mkulima kutoka Moshi DC

Shamba la mfano na wauza pembejeo



"Ni mara ya kwanza tunaalika wasambazaji wa mbegu kwenye kikundi chetu ili kutoa mafunzo ya uzalishaji (kupitia mkuatano wa kutengeneza mausiano ya wadau wa kilimo). " - Mkulima kutoka Moshi DC
(posted on facebook page: @RijkZwaanTanzania)



Mkuatano na wadau wa pembejeo



"Mbinu ya SHEP ni muhimu kwetu katika kutekeleza DADPs zetu" - Afisa wa wilaya kutoka Bumbuli DC
"Nimeanzisha zana za TANSHEP (Utafiti wa Soko na Uunganishwaji wa wadau) kwa wakulima wengine kijijini ukiacha vikundi lengwa vya mradi." - Afisa Ugani kutoka Lushoto DC

Mkakati wa uzalishaji & masoko



Kulingana na matokeo ya utafiti wa soko, wakulima wametengeneza kalenda yao ya upandaji mazao ili kuzalisha kipindi cha bei kubwa. Wakulima wengine walikodisha mashamba ya umwagiliaji kwa pamoja kama kikundi na kuanza uzalishaji wa vitunguu ili kuvuna wakati wa bei kubwa.

Ratiba

